**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA (FUNGU 38, 39, 57) KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

*[Imetolewa chini ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016]*

**MEI,2018**

1.0 UTANGULIZI ........ 1

2.0 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 ........ 3

2.1 Maelezo kuhusu Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa ........ 3

2.2 Matokeo ya Ukaguzi wa Mradi ........ 3

2.3 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 ........ 4

3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 ........ 5

3.1 Uchambuzi wa Mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 ........ 5

3.1.1 Uchambuzi wa Taarifa kuhusu ukusanyaji wa mapato ........ 6

3.1.2 Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina ........ 9

3.2 Mapitio ya utekelezaji wa ushauri wa Kamati ........ 12

4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 ........ 15

4.1 Mpango wa Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2018/ 2019 ........ 15

4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 ........ 17

4.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi ........ 19

5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI ........ 21

6.0 HITIMISHO ........ 25

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019**

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 [Kanuni za Bunge], naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee, lijadili na hatimaye kuidhinisha Bajeti ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kifungu cha 6 (3) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, jukumu la kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ni la Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Aidha, Kifungu cha 7 (1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge kinatoa Mamlaka kwa Kamati zote za Kisekta kushughulikia Bajeti za Wizara inazozisimamia. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ilikutana na Waziri

wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa tarehe 29 Machi, 2018 na kuchambua Bajeti ya Wizara hiyo. Kwa utaratibu wa Kibajeti, Wizara hii inahusisha Mafungu matatu (3) yafuatayo:-

i) Fungu 38- Ngome;
ii) Fungu 39- Jeshi la Kujenga Taifa [JKT]; na
iii) Fungu 57- Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa [Wizara].

Kamati ilipitia na kuchambua kwa kina bajeti za mafungu yote matatu na matokeo ya uchambuzi yanaonekana katika sehemu ya tatu na ya nne ya Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, ili kulisaidia Bunge lako Tukufu kufuatilia ipasavyo utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, pamoja na kuishauri vema Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu nne (4) zifuatazo:-

i) Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo;
ii) Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti na uzingatiaji wa Maoni ya Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;
iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019; na
iv) Maoni na Ushauri wa Kamati.

## 2.0 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

### 2.1 Maelezo kuhusu Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98 (1), Kamati ilitembelea na kukagua Miradi ya Maendeleo iliyopo chini ya Wizara mbili kati ya tatu zinazozisimamia na Kamati yangu ikiwewo Wizara ya Ulinzi na JKT, kuanzia tarehe 14 hadi 21 Machi, 2018 katika Mikoa ya Lindi na Mtwara. Kwa Wizara hii, Kamati ilikagua mradi mmoja tu kwa kuwa hakukuwa na miradi mingine iliyokuwa imetengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 katika Mikoa hiyo.

Mradi uliokaguliwa ni Mradi namba 6103 unaojulikana kama'*Defence Scheme*' na kutekelezwa chini ya Kifungu namba 2004 – '*Estate Management Development Unit'* cha Fungu 57. Mradi huu unahusu ulipaji wa fidia kwa eneo la Ras Mishindo, katika Wilaya ya Kilwa, Mkoani Lindi, lililotwaliwa kwa ajili ya matumizi ya Jeshi la Wananchi Tanzania.

### 2.2 Matokeo ya Ukaguzi wa Mradi

**Mheshimiwa Spika**, katika ziara hiyo, Kamati ilibaini kuwa kutokutolewa kwa fedha za maendeleo ni changamoto inayoukabili utekelezaji wa Mradi huu. Taarifa iliyowasilishwa mbele ya Kamati ilieleza kuwa, tathmini ya gharama za fidia

iliyofanyika Mwaka 2015 kwa ajili ya eneo hilo ilikuwa **Shilingi 3,662,108,122.00**.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa zoezi la ulipaji fidia kwa wananchi lilipaswa kuanza tarehe 01 Novemba, 2015 na kukamilika tarehe 30 Aprili, 2016. Hata hivyo, Kamati ilibaini kuwa fedha hizo hazikuwahi kutolewa licha ya kwamba zimekuwa zikitengwa kwa miaka mitatu mfululizo kuanzia Mwaka wa Fedha 2015/2016 hadi 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika,** kutokutolewa kwa fedha kwa ajili ya kulipa Wananchi fidia, kumecheleweshwa eneo hilo kutwaliwa rasmi kwa ajili ya ujenzi wa Kamandi ya Jeshi la Wanamaji (Navy Military Base) ambapo hatimaye, pamoja na mambo mengine, itajihusisha na shughuli za uvuvi wa bahari kuu; ujenzi wa miundombinu ya matengenezo ya Meli; shughuli za kitafiti na kiuchumi kwa maslahi mapana ya nchi yetu.

## 2.3 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na matokeo ya ziara ya ukaguzi wa mradi unaotekelezwa chini ya Fungu 57 pamoja na maelezo ya Serikali kuhusu mwenendo wa upatikanaji wa fedha za maendeleo kwa Mafungu yote matatu ya Wizara hii, Kamati inatoa maoni kwamba mwenendo wa upatikanaji

wa fedha kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni jambo linalohitaji kuboreshwa zaidi. Aidha, Kamati inasisitiza kuwa, Miradi ya Maendeleo ambayo ni dhahiri kuwa ina tija kwa Taifa kiulinzi, kiutafiti na kiuchumi, utekelezaji wake upewe kipaumbele na uzito unaostahili kibajeti.

## 3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 ilihusu maeneo Makuu mawili. Maeneo hayo ni Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge na uzingatiaji wa maoni na ushauri wa Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati ilijadili na kuchambua mambo yote mawili kwa kina kama ifuatavyo:-

### 3.1 Uchambuzi wa Mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati katika Mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2017/ 2018, ulijielekeza katika makusanyo ya mapato ikilinganishwa na

lengo la makusanyo pamoja na upatikanaji wa fedha za matumizi kwa ajili ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa, hususan fedha za Matumizi Mengineyo (OC) na fedha za Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilizingatia taarifa mbalimbali zilizowasilishwa mbele ya Kamati kwa kipindi cha Oktoba, 2017 na Januari, 2018, na majadiliano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu na za ziada wakati wa vikao vya Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha uchambuzi huo kama ifuatavyo:-

#### 3.1.1 Uchambuzi wa Taarifa kuhusu ukusanyaji wa mapato

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, Wizara ilikadiria kukusanya mapato ya jumla ya **Shilingi 69,706,000.00** kutokana na mauzo ya nyaraka za zabuni. Kiasi hiki ni ongezeko la asilimia 2 ikilinganishwa na makadirio ya makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017. Kamati ilijulishwa kuwa hadi mwezi Machi, 2018, Wizara ilifanikiwa kukusanya jumla ya **Shilingi 57,920,242.00** sawa na **asilimia 83.09** ya makadirio. Aidha kiasi hicho ni ongezeko la **Shilingi**

**27,750,379.00** sawa na **asilimia 92** ikilinganishwa na makusanyo ya Wizara kwa kipindi kama hicho katika Mwaka 2017. Uchambuzi wa Kamati umebainisha Mchanganuo wa makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 01.

**Jedwali Na. 01: Makusanyo ya Wizara kwa Mwaka 2017/2018**

| FUNGU | MAKADIRIO | % YA JUMLA YA LENGO | MAKUSANYO | % YA JUMLA YA MAKUSANYO | % YA LENGO LA MAKUSANYO |
|---|---|---|---|---|---|
| 38 - Ngome | 15,601,000.00 | 22.38 | 21,305,042.00 | 36.78 | 136.60 |
| 39 - JKT | 54,003,000.00 | 77.47 | 36,215,200.00 | 62.52 | 67.00 |
| 57 - Wizara | 102,000.00 | 0.15 | 400,000.00 | 0.7 | 392.16 |
| **JUMLA** | **69,706,000.00** | **100** | **57,920,242.00** | **100** | **83.9** |

**Chanzo: Randama ya Wizara 2018/2019**

**Mheshimiwa Spika**, Katika mchanganuo huo, Kamati imebaini yafuatayo:-

i) Makusanyo katika Fungu 38 – Ngome yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa asilimia 22.38 lakini Taarifa ya Makusanyo ilionesha kuwa Fungu 38 limechangia kwa asilimia 36.78 ya kiasi kilichokusanywa. Aidha, kiasi kilichokusanywa ni

asilimia 136.60 ya lengo lililowekwa. Makusanya hayo yametokana na mauzo ya nyaraka za zabuni na kamisheni zinazotokana na JWTZ kuwa Wakala wa ukusanyaji wa makato ya bima zinazokatwa na wanajeshi kutoka Makampuni mbalimbali ya Bima.

ii) Makusanyo ya Fungu 39 –JKT yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa asilimia 77.47, lakini hali halisi imeonesha kuwa makusanyo ya JKT yamekuwa ni asimia 62.52 ya kiasi kilichokusanywa. Aidha, kiasi kilichokusanywa ni sawa na asilimia 67 ya lengo la makusanyo lililowekwa. Makusanyo hayo yametokana na mauzo ya nyaraka za zabuni, mauzo ya mazao ya bustani, mazao ya mifugo na mazao ya shambani.

iii) Makusanyo ya Fungu 57 – Wizara, yalikusudiwa kuchangia katika lengo la makusanyo kwa asilimia 0.15, lakini taarifa ya Wizara imeonesha kuwa makusanyo ya Wizara yamekuwa ni asilimia 0.7 ya kiasi kilichokusanywa. Aidha, kiasi kilichokusanywa ni sawa na asilimia 392.16 ya

lengo la makusanyo lililowekwa. Makusanyo hayo yametokana na Kodi ya Pango la kantini.

**Mheshimiwa Spika,** ulinganisho huo wa malengo ya makusanyo kwa kila Fungu ikilinganishwa na kiasi kilichokusanywa na kila Fungu, uliiwezesha Kamati kubaini kuwa vyanzo vya uhakika vya mapato vimeiwezesha Wizara hii kuwa na mwenendo mzuri wa makusanyo na ni dhahiri kuwa lengo la makusanyo litakuwa limefikiwa hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2018.

### 3.1.2 Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina

**Mheshimiwa Spika,** Bunge lako Tukufu limekuwa likisisitiza kila Mwaka kuhusu umuhimu wa Serikali kutoa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi ya Serikali. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, upatikanaji wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 kwa kiasi kikubwa ni wa kuridhisha.

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wake, Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kufanya ulinganisho wa fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya matumizi yote ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha

2017/2018 na kiasi kilichotolewa hadi kufikia mwezi Machi, 2018. Uchambuzi huo ulibainisha yafuatayo:-

i) Hadi kufikia Mwezi Machi, 2018 Wizara ilikuwa imepokea **Shilingi 1,149,850,688,197.07** sawa na asilimia 66.63 ya bajeti iliyoombwa. Kati ya fedha hizo asilimia **Shilingi 1,012,482,838,197.07** sawa na asilimia 88 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 137,367,850,000.00** sawa na asilimia 12 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

ii) Kiasi kilichopokelewa na Wizara kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni ongezeko la asilimia 283 ikilinganishwa na Shilingi **35,900,000,000.00** zilizotolewa katika Mwaka wa Fedha 2016/2017.

iii) Fedha kwa ajili ya Bajeti ya Matumizi ya Uendeshaji (OC) ilipokelewa kwa asilimia 143.50 ikiwa ni ongezeko la asilimia 85.7 ikilinganishwa na Shilingi **40,933,904,563.74** zilizopokelewa katika kipindi kama hicho kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017. Ongezeko hili limechangiwa na malipo ya madeni ya Shilingi Bilioni 40 yaliyotolewa chini ya Fungu 38.

iv) Kati ya **Shilingi 137,367,850,000.00** zilizopokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendelo, asilimia 94. 7 ya fedha hizo ni kwa ajili ya Fungu 57- Wizara, asilimia 2.9 kwa ajili ya Fungu 39- Jeshi la Kujenga Taifa na asilimia 2.4 kwa ajili ya Fungu 38- Ngome.

v) Katika fedha zilizoombwa kwa kila Fungu, Fungu 57- Wizara lilipokea asilimia 63.40, Fungu 39- JKT lilipokea asilimia 66.70, na Fungu 38- Ngome lilipokea asilimia 41.25.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na uchambuzi huo, Kamati ina maoni kuwa mwenendo huu wa upatikanaji wa fedha za uendeshaji kwa Mafungu yote matatu ni mzuri na unapaswa kuendelezwa. Aidha, Kamati imeridhishwa na utolewaji wa fedha za maendeleo hususan kwa Mafungu 39- JKT na 57- Wizara. Kamati inaamini kuwa Serikali itaona umuhimu wa kutoa fedha za maendeleo kwa Fungu 38- Ngome kama ilivyofanya katika Mafungu hayo mawili ili kutoathiri ratiba na mpango wa utekelezaji wa miradi muhimu ya maendeleo inayotekelezwa na Fungu hilo.

### 3.2 Mapitio ya utekelezaji wa ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa kupitia na kuchambua Mpango na Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, Kamati ilitoa ushauri katika maeneo kumi na sita (16) yaliyopaswa kuzingatiwa na Serikali kuhusu Bajeti hiyo. Masuala hayo yalihusu mambo mbalimbali ikiwemo yafuatayo:-

i) Serikali kutoa fedha zilizotengwa kwa ajili ya kulipa fidia kwa maeneo yaliyochukuliwa na Jeshi;
ii) Serikali kukamilisha mchakato wa kuandaa Sera ya Ulinzi wa Taifa na marekebisho ya Sheria ya Ulinzi wa Taifa ya 1966, Sura 192;
iii) Serikali kulipa madeni ya Shirika la SUMA JKT Guard Ltd;
iv) Serikali kulipa madeni ya Wizara yaliyohakikiwa ya Wazabuni na Watumishi;
v) Serikali kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa miundombinu katika Mashirika ya Nyumbu na Mzinga; na
vi) Serikali kuliwezesha kibajeti Fungu 39- JKT ili kumudu mahitaji ya kuwezesha Vijana wengi zaidi kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa;

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuliarifu Bunge lako kuwa katika masuala yaliyotolewa ushauri, masuala saba (7) yamezingatiwa kikamilifu, masuala saba (7) yanaendelea kuzingatiwa na masuala mawili (2) hayajazingatiwa kabisa kutokana na ufinyu wa bajeti.

**Mheshimiwa Spika**, miongoni mwa ushauri uliozingatiwa kikamilifu ni kuhusu Fungu 39- Jeshi la Kujenga Taifa kuwezeshwa kibajeti ili kumudu mahitaji ya kuwezesha Vijana wengi zaidi kujiunga na Jeshi hilo. Taarifa ya utekelezaji imeonesha kuwa ushauri huu umetekelezwa ambapo hadi kufikia Mwezi Machi, 2018, Fungu hili lilipokea **Shilingi bilioni nne (4)** sawa na asilimia 66.70 ya bajeti ya maendeleo iliyoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2016/2017, ambapo Fungu hili lilipokea **Shilingi bilioni moja (1)** tu sawa na asilimia 12.5 ya bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kupitia fedha hizo, Jeshi la Kujenga Taifa liliweza kuboresha miundombinu na kujenga majengo mapya katika Kambi tano (5) za Mpwapwa- Dodoma, Makuyuni- Arusha, Itaka- Songwe, Milundikwa na Luwa- Rukwa. Kuboreshwa kwa Kambi hizi ni hatua muhimu katika kuliongezea Jeshi la Kujenga Taifa uwezo wa kuchukua Vijana zaidi wa kujitolea na wale wa mujibu wa Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, mfano wa pili wa utekelezaji wa ushauri ni kuhusu kuongeza kasi ya kulipa madeni ya Wizara yaliyohakikiwa ya Wazabuni na Watumishi wa Umma. Katika Mwaka 2017/2018 Serikali imeendelea kulipa madeni kwa kasi ya kuridhisha ambapo hadi kufikia Mwezi Machi, 2018 Wizara, kwa Mafungu yote matatu ilikuwa imepokea **Shilingi 76,589,540,683.29** kwa ajili ya kulipa madeni ikilinganishwa na kiasi cha **Shilingi 31,628,607,462.47** kilichotolewa katika kipindi kama hicho katika Mwaka wa Fedha 2016/2017.

**Mheshimiwa Spika**, mfano wa ushauri ambao unaendelea kuzingatiwa na Serikali ni kuhusu kukamilisha mchakato wa kufanya marekebisho katika Sheria ya Jeshi la Kujenga Taifa, Sura ya 193. Kamati ilielezwa kuwa JKT limekwishafanya mapitio ya Sheria ambayo yameainisha Vifungu mbalimbali katika Sheria hiyo na Kanuni zake ambavyo vinahitaji marekebisho. Mapendekezo ya marekebisho hayo yamekamilika tayari kwa kuwasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa hatua zinazofuata.

**Mheshimiwa Spika,** mfano wa ushauri ambao haukuzingatiwa kikamilifu ni kuhusu Serikali kutoa **Shilingi bilioni 27.7** zilizotengwa katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 kwa ajili ya kulipa Wananchi fidia katika maeneo yaliyochukuliwa na Jeshi kabla ya Mwaka huo wa fedha kuisha. Hata hivyo,

fedha hizo hazikutolewa na sababu zilizotolewa ni changamoto ya kutopatikana kwa fedha za maendeleo kama zilivyoidhinishwa na Bunge. Taarifa ya Wizara ilionesha kuwa katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Wizara iliidhinishiwa jumla ya Shilingi **bilioni 20,038,820,000.00** kwa ajili kulipa fidia. Hata hivyo, hadi kufikia mwezi Machi, 2018 kiasi cha Shilingi **150,000,000.00** sawa na asilimia 0.74 tu ya fedha zilizoidhinishwa ndio kimetolewa kwa ajili ya kulipa deni la fidia ya eneo la Shule ya Mafunzo ya Awali ya Kijeshi RTS-Kihangaiko katika Wilaya ya Bagamoyo, Mkoa wa Pwani.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia Madaraka ya Bunge yaliyoainishwa katika Ibara ya 63 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa ushauri ambao haujazingatiwa unapaswa kufanyiwa kazi na kuwa sehemu ya ratiba ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

## 4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

### 4.1 Mpango wa Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2018/ 2019

**Mheshimiwa Spika,** ili kujiridhisha na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii, Kamati ilirejea Hati Idhini ya Mgawanyo wa Majukumu ya Wizara za Serikali, Toleo la tarehe 22 Aprili,

2016 na kuoanisha na malengo ya Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kuwa katika kutekeleza majukumu ya msingi manne yaliyoainishwa katika Hati Idhini, Wizara inalenga kuimarisha utendaji kazi na kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake kulingana na Dira na Dhima kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika**, lengo hili limepangwa kufikiwa kwa kutekeleza majukumu tisa (9) ikiwemo kuendelea kuwapatia Vijana wa Kitanzania mafunzo ya Uzalendo, Ukakamavu, Umoja wa Kitaifa na Stadi za Kazi pamoja na kuendeleza utafiti na uhawilishaji wa teknolojia kwa madhumuni ya kuzalisha bidhaa pamoja na kuimarisha na kuanzisha Viwanda.

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wake, Kamati imebaini kuwa majukumu yaliyopangwa yatawezesha ufikiaji wa lengo kwa ufanisi endapo tu Serikali itazingatia Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa kutoa fedha zitakazoidhinishwa na Bunge kwa ukamilifu na kwa wakati.

## 4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mafungu yote matatu (38, 39 na 57) inategemea kukusanya mapato ya jumla ya **Shilingi 75,420,100.00**. Kiasi hiki ni sawa na ongezeko la asilimia 8 ikilinganishwa na kiasi kilichopangwa kukusanywa katika Mwaka wa Fedha 2017/2018. Mchanganuo wa lengo hilo la makusanyo unaonekana katika Jedwali Na. 2 la Taarifa hii.

**Jedwali Na. 02 : Mchanganuo wa Mapato**

| **Fungu** | **Makadirio** | | **Asilimia ya lengo la Wizara** |
|---|---|---|---|
| 38 - Ngome | Shilingi | 17,317,100.00 | 22.96 |
| 39 - JKT | Shilingi | 56,903,000.00 | 75.45 |
| 57 - Wizara | Shilingi | 1,200,000.00 | 1.59 |
| **JUMLA** | Shilingi | **75,420,100.00** | **100.00** |

**Chanzo: Randama ya Wizara 2018/2019**

Kwa uchambuzi huo, Kamati imebaini yafuatayo:-

i) Lengo la Makusanyo kwa Mafungu yote ya Wizara limeongezeka kwa asilimia 8 ikilinganishwa na lengo la makusanyo kwa Mwaka wa Fedha unaoisha. Jambo hili ni la kupongeza kwani kwa Mwaka wa fedha 2017/2018

lengo hilo liliongezeka kwa asilimia 1.9 ikilinganishwa na lengo la Makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017;

ii) Ongezeko la lengo la Makusanyo kwa Mwaka wa fedha 2018/2019 limezingatia ongezeko la makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 ambapo lilifikiwa kwa asilimia 83.09 hadi robo ya tatu ya Mwaka wa Fedha unaoishia.

iii) Fungu 38 – Ngome, linategemewa katika makusanyo kwa asilimia 22.96 ambapo Mwaka 2016/2017 lilitegemewa kwa asilimia 22.38.

iv) Fungu 39 – JKT, linategemewa katika makusanyo kwa asilimia 75.45 ambapo Mwaka 2017/2018 lilitegemewa kwa asilimia 77.47.

v) Fungu 57- Wizara, linategemewa kwa makusanyo kwa asilimia 1.59 wakati Mwaka 2017/2018 lilitegemewa kwa asilimia 0.15.

**Mheshimiwa Spika**, kwa maelezo hayo, Kamati inaipongeza Wizara kwa kuzingatia maoni ya Kamati kuhusu lengo la ukusanyaji wa mapato kwa kuzingatia uhalisia wa makusanyo yanayopatikana.

## 4.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi

**Mheshimiwa Spika**, maelezo ya Waziri wa Ulinzi mbele ya Kamati yalionesha kuwa katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inayoombwa kwa Mafungu yote matatu ni Shilingi **1,910,722,891,000.00.** Kati ya Fedha hizo, Shilingi **1,676,722,891,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **234,000,000,000.00** ni kwa ajili ya kugharamia Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, ili kukidhi Masharti ya Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilifanya uchambuzi wa makadirio hayo kwa kupitia Kasma (Items), Vifungu (Subvotes) na Mafungu (Votes) yote ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa na kutekelezwa kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. Katika uchambuzi huo, Kamati ilibaini yafuatayo:-

i) Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 imeongezeka kwa **Shilingi 185,205,073,654.00** sawa na ongezeko la asilimia 1 ikilinganishwa na bajeti ya Mwaka wa Fedha 2017/2018. Pamoja na ongezeko hilo, Kamati imebaini kiasi kinachoombwa bado ni kidogo ikilinganishwa na mahitaji halisi ya Wizara ambayo ni **Shilingi 2,877,842,169,617.00.**

ii) Asilimia 8 ya bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na asilimia 92 ya bajeti ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Uwiano huu kwa fedha za maendeleo umepungua ikilinganishwa na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2017/2018 ambapo asilimia 12.7 ya bajeti ilikuwa ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na 87.3 ilikuwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

iii) Kiasi cha fedha kinachoombwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kimeongezeka kwa asilimia 6. Fedha hizi zimeongezeka katika Fungu 57- Wizara, hususan katika kuendeleza utafiti na uzalishaji katika Mashirika ya Nyumbu na Mzinga;

iv) Kati ya **Shilingi 234,000,000,000.00** zinazoombwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, asilimia 94 ni kwa ajili ya Fungu 57- Wizara, asilimia 3.4 ni kwa ajili ya Fungu 38- Ngome, na asilimia 2.6 ni kwa ajili ya Fungu 39- JKT.

**Mheshimiwa Spika**, maelezo hayo yametokana na uchambuzi wa Kamati baada ya kupitia Randama za Mafungu matatu ya Wizara hii na kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Naomba Bunge lako tukufu lipokee maelezo hayo yatakayosaidia

majadiliano kuhusu hoja iliyowasilishwa na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa mapema leo hii.

## 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia taarifa ya utekelezaji wa maoni ya Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 sambamba na majadiliano ya kina kuhusu Makadirio ya Mapato, Mipango na Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na JKT kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 ikilinganishwa na Dhima ya Wizara ya kulinda uhuru, maslahi na mipaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuataao:-

i) Serikali ione umuhimu wa kuongeza ukomo wa bajeti ya Wizara hii kulingana na mahitaji yake halisi ili kuliongezea Jeshi letu uwezo wa kiutendaji. Mahitaji halisi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 ni **Shilingi 2,877,842,169,671.00** ambapo ukomo wa bajeti uliowekwa ni **Shilingi 1,910,722,891,000**.

ii) Kwa kuwa bajeti inayoidhinishwa hususan ya maendeleo imekuwa ikitolewa kwa kiwango kidogo jambo linaloathiri utekelezaji wa ratiba ya Miradi ya Maendeleo vilevile kupoteza uaminifu kwa wazabuni wanaotoa huduma mbalimbali, Serikali ione umuhimu wa kutoa

fedha zote za maendeleo ambazo zilitengwa katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 hususan kwa Fungu 38 ambalo lilipokea asilimia 41.25 tu ya fedha zilizotengwa.

iii) Kamati inapongeza juhudi za SUMA JKT GUARD LTD katika kukusanya madeni ya huduma za ulinzi kutoka kwa wadaiwa sugu ambapo madeni yaliyokusanywa hadi kufikia Mwezi Mei, 2018 ni **Shilingi 3,451,105,387.00 kati ya Shilingi 4,056,952,232.00**. Miongoni mwa Wizara na Taasisi zinazodaiwa ni pamoja na:-

a) Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi;
b) Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii; Jinsia, Wazee na Watoto;
c) Wizara ya Fedha na Mipango;
d) Wizara ya Viwanda na Biashara;
e) NIDA- Dar es Salaam; Chuo cha Madini-Nzega;
f) Stamigold- Biharamuro; na
g) Chuo cha Serikali za Mitaa- Hombolo.

Kamati inasisitiza Wizara na Taasisi ambazo zinadaiwa zilipe madeni hayo ili kutoathiri utendaji wa Shirika la SUMA JKT GUARD. Aidha, Kamati inasisitiza kuwa, ili

kupunguza tatizo sugu la madeni, SUMA JKT GUARD ijielekeze na kujikita katika kazi zenye zabuni ya ulinzi.

iv) Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuhakikisha kwamba wadaiwa sugu waliokopa matrekta kutoka SUMA JKT wanarejesha madeni hayo ambayo kwa sasa ni takribani Shilingi Bilioni 40. Miongoni mwa wadaiwa sugu ni pamoja na Halmashauri za Wilaya za Kasulu, Kibaha na Geita.

v) Serikali iboreshe maslahi ya walinzi wa SUMA JKT GUARD kwa mujibu wa Sheria zilizopo ili yaendane na hali halisi ya kiuchumi;

vi) Kwa kuwa lengo la Serikali ni kuongeza idadi ya Vijana wengi kujiunga na JKT kwa mujibu wa Sheria na Kujitolea, Kamati inaishauri Serikali kutoa fedha za maendeleo **Shilingi Bilioni 2** ambazo hazijatolewa kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu na ujenzi wa makambi mapya ya JKT ili Vijana zaidi wachukuliwe katika Mwaka wa Fedha 2018/2019.

vii) Kamati inaendelea kuishauri Serikali kutoa fedha zote za maendeleo zinazoidhinishwa kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya Mashirika ya Nyumbu- Kibaha

na Mzinga- Morogoro ili kufanikisha shughuli za utafiti na uzalishaji wa bidhaa kwa ajili ya matumizi muhimu. Kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, Shirika la Mzinga lilipokea **Shilingi Bilioni 2.5** sawa na asilimia 38.46 ya **Shilingi Bilioni 6.5** zilizoidhinishwa kwa ajili ya uzalishaji wa bidhaa muhimu. Aidha, Shirika la Nyumbu lilipokea **Shilingi Bilioni 1.5** sawa na asilimia 7.50 ya Shilingi **Bilioni 20** zilizoidhinishwa kwa ajili ya utafiti. Ushauri huu ulitolewa na Kamati katika Bajeti ya Wizara ya Mwaka 2017/2018 lakini haukuzingatiwa kikamilifu.

viii) Serikali itoe fedha kiasi cha **Shilingi 19,888,820,000.00** ambazo hazijatolewa katika Mwaka 2017/2018 kwa ajili ya kulipa fidia katika maeneo yaliyotwaliwa kwa matumizi ya Jeshi. Aidha, kipaumbele kitolewe kwa eneo la Ras Mishindo katika Wilaya ya Kilwa, Mkoa wa Lindi, kutokana na umuhimu wake kiuchumi na kiulinzi ambapo fidia inayodaiwa ni **Shilingi 3,662,108,122.00**. Fedha hizo zimekuwa zikitengwa tangu Mwaka wa Fedha 2015/2016 lakini hazijawahi kutolewa jambo ambalo linachelewesha utekelezaji wa mradi huo muhimu.

ix) Kwa kuwa Kamati imekuwa ikiishauri Serikali mara kwa mara tangu Bunge la Tisa kuhusu kukamilisha mchakato

wa Sera ya Ulinzi wa Taifa; na kwa kuwa mchakato huo unasubiri maoni ya Rasimu ya Sera hiyo kwa Upande wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Kamati inaishauri Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais, kuwasilisha maoni hayo haraka ili kukamilisha Sera hiyo. Pamoja na mambo mengine, uwepo wa Sera hiyo utawezesha marekebisho ya Sheria ya Ulinzi wa Taifa ya Mwaka 1966, Sura 192 ili iendane na wakati, Mifumo ya Utawala na mahitaji ya sasa ya kisheria katika Sekta ya Ulinzi.

x) Kwa kutambua mchango muhimu wa Viongozi Wastaafu wa Jeshi katika masuala ya ulinzi na usalama, Kamati inaishauri Serikali kulipa stahili za majenerali wastaafu kama zinavyoidhinishwa kila Mwaka. Kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 **Shilingi 3,950,400,000.00** zilitengwa kwa ajili ya shughuli hiyo hata hivyo hadi kufikia mwezi Machi, 2018, ni **Shilingi Bilioni 1** tu sawa na asilimia 25 iliyokuwa imetolewa.

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuwasilisha Taarifa hii. Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha

kukamilika kwa taarifa hii. Naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Mussa Azzan Zungu, Mb- MWENYEKITI
2. Mhe. Salum Mwinyi Rehani, Mb- MAKAMU MWENYEKITI
3. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb
4. Mhe. Mussa Hassan Mussa, Mb
5. Mhe. Prosper J. Mbena, Mb
6. Mhe. Mhe. Victor Kilasile Mwambalaswa, Mb
7. Mhe. Fakharia Shomari Khamis, Mb
8. Mhe. Joram Ismael Hongoli, Mb
9. Mhe. Joseph Michael Mkundi, Mb
10. Mhe. Zacharia Paulo Issaay, Mb
11. Mhe. Cosato David Chumi, Mb
12. Mhe. Mboni Mohamed Mhita, Mb
13. Mhe. Shally Joseph Raymond, Mb
14. Mhe. Fatma Hassan Toufiq, Mb
15. Mhe. Sebastian Simon Kapufi, Mb
16. Mhe. Bonna Mosses Kaluwa, Mb
17. Mhe. Silafu Jumbe Maufi, Mb
18. Mhe. Ruth Hiyob Mollel, Mb
19. Mhe. Dkt. Suleiman Ally Yussuf, Mb
20. Mhe. Masoud Abdalla Salim, Mb
21. Mhe. Sophia Hebron Mwakagenda, Mb
22. Mhe. Janeth Maurice Massaburi, Mb
23. Mhe. Augostino Manyanda Masele, Mb
24. Mhe. Almasi Athuman Maige, Mb
25. Mhe. Eng. Gerson Hosea Lwenge, Mb

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Ulinzi na JKT Mhe. Dkt. Hussein Mwinyi (Mb) kwa ushirikiano wake mzuri katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya Kikanuni ya Kamati. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu Ndugu Florens Turuka pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano wao.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge. Aidha, nawashukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athumani Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Bi. Angelina Sanga na Makatibu wa Kamati hii Ndg. Ramadhan Abdallah na Bi. Grace Bidya wakisaidiwa na Bi. Rehema Kimbe, kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati**.**

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na JKT kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Mussa Azzan Zungu, **Mb**

**MWENYEKITI**
**KAMATI YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA**
14 Mei, 2018